LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# TAMKO KUKEMEA NDOA ZA UTOTONI

## Utangulizi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinasikitika kutokana na mjadala ulioibuka hivi karibuni kuhusu umri wa mtoto wa kike kuolewa na kutokurekebishwa kwa sheria ya ndoa. Mijadala hii inapingana na sheria kwani baada ya Mahakama ya Rufaa kuamua shauri la Rebeca Gyumi umri wa mtoto wa kike kuolewa Tanzania ni miaka 18. Ikumbukwe kuwa maamuzi ya Mahakama ni sheria lazima yaheshimiwe na watu wote ikiwepo Serikali. Mijadala hiyo imekuwa ikiibuka sehemu mbalimbali katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ambapo imekuwa ikipendekezwa kuwa hakuna haja ya kuifanyia marekebisho sheria ya ndoa inayoruhusu umri wa ndoa kuwa miaka 14 kwa amri ya ,ahakama na 15 kwa ridhaa ya wazazi katika vifungu vyake vya 13 na 17 vya sheria ya ndoa ya mwaka 1971.

Kwa mujibu wa mijadala hiyo mtoto mwenye umri wa miaka 11, 12, au 13 aliyeingia kipindi cha balehe aruhusiwe kuolewa kwa amri ya Mahakama kwa kuzingatia vielelezo vya kimazingira ikiwemo afya, Imani, mila na desturi za jamii husika. Mijadala hiyo imeshauri kuwa kama binti hajaweza kuendelea na masomo, asipoingia kwenye ndoa anaweza kupata mimba kabla ya ndoa na hivyo kuleta madhara zaidi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinalaani vikali mijadala kama hii na mapendekezo kama haya kwani yanarudisha nyuma juhudi za kumkomboa mtoto wa kike dhidi ya imani, mila na desturi kandamizi.

Ndoa za utotoni ni tatizo kubwa nchini Tanzania linalo sababisha wasichana kutotimiza ndoto zao hasa za kielimu. Ndoa hizi mara nyingi husababishwa na hali duni za kimaisha, mila na desturi zilizopitwa na wakati, ukeketaji, ukosefu wa elimu juu ya madhara ya ndoa za utotoni n.k. Kutokana na takwimu za TDHs za mwaka 2015/16 zinaonesha wasichana 2 kati ya wasichana 5 wanaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Hii ni hatari sana na inapelekea idadi kubwa ya wasichana wadogo kupoteza malengo yao, haki zao za msingi na hata wengine kupoteza maisha.

Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuweka umri wa chini wa ndoa kuwa miaka 18, kwani kuna nchi nyingi ambazo umri wa ndoa ni miaka 18 na kuendelea. Mfano wa mataifa hayo ni pamoja na Saudi Arabia ambapo ndoa katika umri chini ya miaka 18 yatakiwa ipitishwe na Mahakama, Algeria ni miaka 18, Iraq ni miaka 18, Jordan miaka 18, Morocco ni miaka 18, pamoja na

**Board of Directors:**
**Hon. Chief Justice (Retired) Barnabas A. Samatta - Chairperson, Ms. Anastazia Rugaba - Vice Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Rebeca Z. Gyumi - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Josephine A. Zimba - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki – Member, Dr. Ally Hussein Laay - Member**

Tunisia miaka 20. Nchi hizi ni nchi zinazoongozwa na sheria za dini ya Kiislamu. Ushahidi huu unatuaminisha kuwa katika mazingira yoyote umri wa ndoa unaweza kuwa miaka 18 au zaidi na usiathiri maendeleo ya nchi, imani mbalimbali na taratibu zilizopo.

## Sheria za Tanzania na Mikataba ya Kimataifa.

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu ndoa kwa mtoto wa kike katika umri wa miaka 14 na miaka 15 kabla ya kubatilishwa na mahakama. Sheria hiyo inapingana na sheria nyingine ikiwemo sheria ya Mtoto inayotaka mtoto kutojihusisha na vitendo vya kingono hadi atakapofikisha umri wa miaka 18, sheria ya kanuni ya adhabu inayotambua kosa kufanya mapenzi na mtoto chini ya miaka 18 pamoja na sheria ya mikataba inayotambua umri wa kuingia mikataba ni miaka 18. Vifungu hivyo pia vinapingana na mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya haki za mtoto ambayo Tanzania imeridhia. Mikataba hiyo ni pamoja Mkataba wa Kimataifa wa haki ya Mtoto (CRC) pamoja na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Kuendelea kukumbatia vifungu hivi ni kukinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania inayopinga ubaguzi pamoja na mikataba ambayo Tanzania imeridhia.

Nguzo muhimu ya kutokomeza ndoa za utotoni, ni kuwa na mfumo imara wa Sheria unaoweka umri wa chini wa kuoa na kuolewa kwa wavulana na wasichana kuwa sawa na kwa umri wa miaka 18 kwani ndio umri wa mtu mzima kwa Tanzania. Kuweka umri wa chini kuwa miaka 18 kunaendana na malengo na viwango vya kimataifa na kikanda kwenye masuala ya haki za binadamu. Pia Sheria ya mfano ya Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika ya kukomesha ndoa za utotoni (SADC Model Law on Eradicating Child Marriages), imeweka wazi miaka 18 kuwa umri wa chini wa kuoa/kuolewa.

## Maamuzi ya Mahakama pamoja na Kamati

Mahakama Kuu ya Tanzania katika shauri la Rebeca Gyumi iliamuru Serikali kufanya marekebisho ya sheria ya ndoa ndani ya mwaka mmoja na kusahihisha vifungu vya kibaguzi vya 13 na 17 na kuweka miaka 18 kama umri wa chini unaostahili kwa ndoa kwa wavulana na wasichana. Uamuzi huu wa Mahakama Kuu ulidhibitishwa na Mahakama ya Rufaa baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukata rufaa. Mahakama katika kujielekeza kwenye maamuzi ya miaka 18 ilizingatia mambo mengi ikiwemo sababu za kisheria na kisera tulizozitaja hapo juu. Kwa hiyo, serikali inawajibu pia wa kutekeleza maelekezo ya Mahakama kuhusu umri wa chini wa ndoa.

Pia katika shauri lilifunguliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu dhidi ya Serikali ya Tanzania katika Kamati ya Wataalamu ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto, iliyomalizika mwaka jana, Serikali ya Tanzania ilimariwa na Kamati hiyo kuchukua hatua stahili kuondoa kabisa ndoa za utotoni na mila nyingine kanadamizi kwani zinaathiri maendeleo ya mtoto wa kike kwa kuhakikisha wanatatua visababishi ikiwemo ubaguzi, umasikini na mila na sedturi zilizopitwa na wakati.

## Madhara ya ndoa za Utotoni

Ndoa za utotoni zimeendelea kuleta madhara makubwa kwa watoto wa kike na taifa kwa ujumla na kuendelea kulisababishia taifa hasara kubwa. Baadhi ya athari hizi ni kama vile kupoteza fursa za elimu na ujuzi wa kazi, kupata maambukizo ya virusi vya ukimwi (VVU) au magonjwa ya zinaa (STD), kunyanyasika kisaikolojia, kimwili, na kijinsia kupitia ukatili ambapo mabinti wengi wanapitia, kuyumba kiuchumi na kudumu katika umasikini, vifo vya watoto wachanga na watoto wa kike pindi wanapojifungua kwa kuwa viungo vyao vya uzazi bado havijakomaa, kuongezeka vifo vya wajawazito, kulipa hasara Taifa katika kutatua changamoto zinazotokana na ndoa za utotoni.

## Mapendekezo

Kutokana na hayo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza;

i. Umri wa mtoto kuolewa Tanzania ni miaka 18 kulingana na kesi ya Rebeca Gyumi baada ya muda waliopewa Serikali kurekebisha sheria kuisha.

ii. Serikali irekebishe vifungu vya 13 na 17 vya sheria ya ndoa ilikuonyesha nia njema (*political will*) na kuondokoa upotoshaji wa umri wa ndoa kwa watanzania.

iii. Mamlaka na wadau watumie nafasi zao kuweza kuunga juhudi kupambana dhidi ya mila kandamizi zinazomnyima mtoto wa kike haki zake za msingi

iv. Wadau wajiepushe na matamko yanayorudisha nyuma juhudi za kumkomboa mtoto wa kike

v. Jamii zitambue mtoto wa kike ana haki za msingi na hivyo haki zake zilindwe na wajiepushe na kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati kwani kufanya hivyo kutaendelea kumkandamiza mtoto wa kike.

vi. Serikali iondoe sheria kandamizi zote na kuhakikisha ulinzi wa mtoto kisheria unapatikana katika sheria zote za msingi katika ulinzi wa mtoto.

**Imetolewa leo tarehe 28.03.2023**

..................................

**Dr. Anna Henga (Wakili)**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**